**HALMASHAURI YA WILAYA YA USHETU**

**KATA YA UYOGO**

**SHULE YA MSINGI NSUNGA**

**MTIHANI WA MUHULA WA PILI NOVEMBA 2025**

**SOMO:KISWAHILI DARASA LA V**

**JINA…………….……………………………………………………………………………………………….**

**SEHEMU A:(ALAMA 20)**

**UFAHAMU WA KUSIKILIZA**

**1.Sikiliza kwa makini habari itakayosomwa na msimamizi kisha jibu kipengele cha (i)-(v) kwa kuchagua herufi ya jibu sahihi**

i)Wanyama uliosomewa katika habari walikuwa wanaishi katika kijiji cha......(A)Hewanii (B)Hewa (C)Hawani (D)Hewani (E)Hayani ( )

ii)Ni kitu gani kilisababisha kijiji cha wanyama hao kuwa na maendeleo duni? (A)Walikuwa wachache (B)Kwasababu ya unyama wao (C)Uvuvi (D)Uvivu (E)Kutojua kusoma kuandika na kuhesabu ( )

iii)Uongozi uliokuwepo unatupiwa lawama gani? (A) Hawakujua uongozi (B) Haukuhamasisha kupiga domo (C) Hawakufanya mkutano(D) Haukuona tatizo (E)Haukuhamasisha wanyama kufanya kazi kwa bidii ( )

iv)Ni nani aliyeitisha mkutano kujadili swala la maendeleo katika Kijiji? (A) Mfalme (B) Sokwe (C) Uongozi (D) Wanyama (E) Wote waliafiki ( )

v)Wanyama wote waliafiki.Sentensi hii ina maana gani? (A)Walivurugana (B)Walikubaliana (C) Walilandana (D) Walilaumiana (E) Walichekana ( )

**2.Katika kipengele cha (i)-(x) chagua jibu sahihi kisha andika herufi yake katika kisanduku ulichopewa**

i)Jana.......kitabu kinachoelezea utii wa watoto kwa wazazi na walimu. (A)Nimesoma (B)Nilisoma (C) Nitasoma (D) Utasoma (E) Anasoma ( )

ii)Amina .........ujumbe aliopewa na mwalimu wake. (A)Ameletewa (B)Amewasilisha (C)Amewakilisha (D)Amefanikisha (E) Amepeleka ( )

iii)Wanaimba kabla ya kuondoka shuleni.Katika neno “Wanaimba”,silabi inayoonesha nafsi ni ipi? (A) wa (B) na (C) imb (D) a (E) ba ( )

iv)Hali ya mazoea ya kufanya jambo fulani huitwaje? (A)Dharura (B)Tumbuiza (C) Sema (D) Tabia (E) Hiyana ( )

v)Mtu hodari asiyeogopa anaitwaje? (A)Jambazi (B)Jangili (C)Jasiri (D)Jeuri (E)Njemba( )

vi)Andika neno ambalo ni tofauti na maneno mengine kati ya maneno yafuatayo (A)Gurudumu (B)Mkunga (C)Usukani (D)Gia (E)Breki ( )

vii)Neno “ZUNGUKA” lina irabu ngapi? (A)2(B)3(C)4(D)5(E)6 ( )

viii)Baba ana viatu vizuri.Neno “vizuri” ni aina gani ya neno? (A)Kitenzi (B)Kivumishi (C)Kielezi (D)Nomino (E)Kiwakilishi ( )

ix)Chakula kitaletwa kutoka mjini.Sentensi hii ipo katika wakati gani? (A) Uliopo (B)Ujao (C)Uliopita (D)Mazoea (E)Mtimilifu ( )

x)Kinyume cha neno duni ni(A)Imara(B)Dhaifu(C)Hohehahe(D)Dunia(E)Zaifu ( ) **3.Oanisha maneno ya kifungu A na yale ya kifungu B ili kuunda maana kamili**

| KIFUNGU A | JIBU | KIFUNGU B |
|---|---|---|
| i)Akufaaye kwa dhiki | | A)Tembea haraka |
| ii)Adui tumemzingira lakini hatumuwezi | | B)Aangalie asianguke |
| iii)Piga mguu | | C)Moto |
| iv)Kupambana kwa nguvu zote mpaka mwisho | | D)Kufa kishujaa |
| v)Ajidhaniaye amesimama | | E)Ndiye rafiki wa kweli |

**SEHEMU B:ALAMA (20)**

**4.Panga sentensi kwa kuzipa herufi A,B,C,D,E ili zilete mpangilio mzuri**.

i)Wakati wa likizo Kapongo humsaidia mama yake shughuli mbalimbali ( )

ii)Pia humsaidia kuuza genge la mali mbichi ( )

iii)Kapongo anaishi na mama yake katika kijiji cha Msuke ( )

iv)Humsaidia kazi za shambani pamoja na za nyumbani ( )

v)Anasoma shule ya msingi Kiponda iliyopo wilaya ya Kasulu ( )

**5.Jaza nafasi zilizoachwa wazi katika sentensi zifuatazo;**

i)Sauna ni kifungua mimba katika familia yao.Je,Sauna ni mtoto wa ngapi kuzaliwa?.............

ii)Wanafunzi wanafanya usafi wa mazingira kwa pamoja.Neno "wanafanya" lipo katika wakati gani?......................................................

iii)Dada anafua nguo kwa kutumia <u>karai</u>.Kisawe cha neno lililopigiwa mstari ni kipi?............................................

iv)Watoto hupenda sana kucheza kuliko kusoma.Je sentensi hii ipo katika hali gani?.........................................................

v)Wanafunzi walitegua kitendawili kwa kusema “siafu” Je,kitendawili hicho kilitegwaje?.....................................................................

**SEHEMU C:UFAHAMU (ALAMA 10)**

**6.Soma habari hii kisha jibu kipengele cha (i)-(v)**

Ususi ni kazi ya sanaa inayotumia nywele halisi,nywele za bandia maarufu kama rasta,Kamba za pastiki,kamba za vitambaa,kamba zitokanazo na mimea mbalimbali,nyuzi na majani.Mimea inayozalisha kamba za aina hii huota katika maji na nchi kavu.Aina hii ya mimea ni pamoja na migomba,miyaa,miyombo,Plastiki,vitambaa,mimea na majani hutoa nyuzinyuzi ambazo hutumika kusokotea vitu mbalimbali katika ususi.Misokoto hii hutumika katika kusokotea vitu mbalimbali kama vile mapambo ya ukutani,kata za mezani,mazulia,mikeka, vikapu,nyungo,kawa na vingine vingi.Kazi ya sanaa ya ususi hujihusisha pia na usukaji wa nywele unaotumia nyuzinyuzi katika mitindo mbalimbali.

**MASWALI**

i)Habari hii inahusu nini?.........................................................................

ii)Nywele za bandia kwa jina jingine hujulikana kama.........................................

iii)Mimea inayozalisha kamba zinazotumika kwa ususi huota maeneo gani?...................................................................

iv)Taja mimea miwili inayotoa kamba kwaajili ya ususi......................................na......................................

v)Zaidi ya ususi wa nywele ni kitu gani kingine unaweza kusuka kwa kusokotea?..........................................................................................